# 12 KUMI KUTOA MOJA NI SIFURI 10-1=0

**10-1 unapata nini? Kule shule tulifundishwaje?** Huenda ukasema ni 9, lakini Mungu anasema ya kwamba 10-1=0. Je, sayansi iliyo sahihi imekuwa isiyo sahihi? Hapana, Mungu analo jibu sahihi, ni hesabu katika kipimo kingine.

Wala hili sio jambo lisilo muhimu sana! Furaha yetu binafsi pamoja na ile ya familia, pamoja na ustawi wa mataifa, hutegemea jambo hili. Hata wokovu wetu wenyewe upo mashakani. Mungu hakubaliani na dini ya kubembelezana. Watu wamezowea kubembelezana, na dini za kisasa zinajaribu kufanya masikilizano na Mungu. Wanapenda dini zenye misisimko pasipo kuwajibika, pasipo na utii kwa Mungu, pasipo na kanuni. Wanatarajia kwamba Mungu atafanya mapunguzo na kuamini ya kwamba kama wakishika nyingi katika zile amri basi yatosha kwao kukubaliwa mbele za Mungu. Wanazichukulia zile amri kama vile waonavyo wao wenyewe.

## *HEBU NA TUHESHIMU KILE MUNGU ALICHOSEMA*

**1. Je, Biblia inasemaje juu ya mtu yule anayeikataa yo yote katika zile Amri Kumi? Yakobo 2:10-12.**

_______________________________________________

**2. Je, Mungu anasemaje juu ya wale ambao wanadhani ya kwamba wamekuwa ni Wakristo wazuri lakini hawazishiki amri Zake? 1 Yohana 2:3, 4.** _______________________

**3. Je, anasemaje juu ya wale wanaoipanga dini kama vile wapendavyo na kubadili baadhi ya zile amri? Mathayo 15:9.** _______________________

a) Mungu hajaruhusu badiliko lo lote katika sheria Yake. Kumbukumbu 4:2; Muhubiri 3:14.

b) Hapana hata badiliko dogo liwezalo kufanywa. Mathayo 5:17-19.

c) Hapajawa na sababu ya kubadili kitu cho chote katika ile sheria. Ile sheria ni kamilifu. Zaburi 19:7.

## *LAKINI NI JUU YA SHERIA GANI AMBAYO MAFUNGU HAYA HUELEKEZA?*

*ZILE AMRI KUMI, HAKIKA KAMA ZILIVYOANDIKWA KWA CHANDA CHA MUNGU.*

**4. Ile amri ya kwanza inakataza nini? Kutoka 20:3.**

_______________________________________________

*AJua pamoja na sayari nyinginezo zilikuwa zikiabudiwa huko nyuma; na hata sasa watu katika nchi nyingine huabudu wanyama; kwa mfano, ng'ombe hufikiriwa kuwa ni watakatifu kule India. Hivi sasa, tunayo miungu ya kisasa. Kitu cho chote ambacho tunachokiona kuwa ni muhimu kuliko Mungu kinakuwa ni mungu kwetu; kwa mfano, kuishi ili kula badala ya kula ili kuishi (Wafilipi 3:19) ama tunapotoa kipaumbele kwenye starehe, michezo, zawadi, n.k. (Mathayo 10:37), inakuwa ni aina ya ibada ya miungu.*

**5. Je, ile amri ya pili inakataza nini? Kutoka 20:4 -6.**

_______________________________________________

*a) Hapa pana sababu ya jambo hili. Kumbukumbu 4:15, 16.*

*b) Yohana 4:24. Mungu anatutaka tumwabudu Yeye katika* _______________________

*c) Je, Biblia inasemaje juu ya ibada ya miungu? Isaya 44:9, 10, 18, 19.*

**6. Je, ile amri ya tatu inakataza nini? Kutoka 20:7.**

_______________________________________________

a) Mungu ni mtakatifu Naye anataka kwamba tulichukue jina Lake kwa kicho. Katika Mathayo 5:34-37

tunaona ya kwamba amri hii inakataza pia ________________________________. Isipokuwa tu kiapo cha kisheria (mahakamani).

b) Je, kutatokea nini kwa wale wanaosema maneno ya ovyo? Mathayo 12:36.

**7. Ile amri ya nne inatuamuru tufanye nini? Kutoka 20:8-11.**

_______________________________________________________________________________

*Ni lazima tufanye kazi katika siku sita za kwanza za juma na kupumzika katika siku ya saba, ndio Sabato. Ni kumbukumbu ya uumbaji, nayo inapasa kuwekwa wakfu kwa ajili ya ibada. Ni kwa ajili ya faida yetu wenyewe. Marko 2:27.*

*Huenda masomaji alipata kujifunza ya kwamba amri ya tatu inasema, "zitakaseni sikukuu." Ama ni kwa sababu gani kuna tofauti juu ya namna ambavyo zile amri zinavyofundishwa? Wale wanaofundisha amri hii kwa namna hii huiruka ile amri ya pili na kuigawanya ile amri ya mwisho iwe ni mbili, ili zipatikane 10. Kuadhimisha "sikukuu" sio sawa na kuiadhimisha siku fulani mahususi. Mungu hajamwidhinisha mwanadamu ye yote kuibadili sheria Yake. Tunapasa kuipokea kama vile ilivyoandikwa katika Biblia.*

**8. Je, ni nani tupasao kuwaheshimu kwa kulingana na amri ya tano? Kutoka 20:12.**

_______________________________________________________________________________

**9. Amri ya sita inaeleza, "Usiuwe." Kutoka 20:13. Amri hii ina maana gani kwa kulingana na mafundisho ya kiroho ya Kristo?**

*Hatuna haki ya kuondoa uhai wa mtu ye yote, hata wetu sisi wenyewe.*

*a) Mathayo 5:38, 39, 43-45. Wapendeni ____________________________________.*

*Yesu Kristo alililifafanua juu ya maana ya kiroho ya amri hii, ambayo inakataza kushiriki katika vita, ambayo ni mauaji makubwa; ni kinyume na mafundisho Yake.*

*b) Mathayo 5:21, 22; 1 Yohana 3:15. Kumchukia mtu, kuapa ama kuweka kinyongo pia ni uvunjaji wa amri hii.*

*c) 1 Wakorintho 3:16, 17. Tusizihalifu zile sheria za _______________________________*

**10. Amri ya saba inasema, "Usizini." Kutoka 20:14.**

*Amri hii inalinda umoja wa familia. Mahusiano yo yote ya kindoa nje ya ndoa Mungu ameyakataa.*

*a) Je, Yesu alisema nini juu ya kutazama na kuwaza kwa kutamani? Mathayo 5:27, 28.*

_______________________________________________________________________________

*b) Je, ni halali kwetu kuangalia matukio ya ghasia na ukafiri wa kindoa hata kama sio kitu halisi? Wafilipi 4:8. ______________________________________________________*

**11. Amri ya nane inakataza nini? Kutoka 20:15.**

_______________________________________________________________________________

*Hii inajumuisha namna zote za wizi, ukiwa mkubwa ama mdogo; kama vile kuteka vitani, utumwa, kutokuwa mwaminifu katika biashara, kuchanganya bidhaa, vipimo vya uongo, kutumia nafasi ya kutofahamu ama udhaifu wa mtu mwingine, kuharibu mvuto wa mtu, kutowajibika kazini, mishahara isiyostahili, kwa ujumla ni kila kitu kilicho katika tendo lisilo la uaminifu.*

**12. Amri ya tisa inasema, "Usimshuhudie jirani yako uongo." Kutoka 20:16. Ni nani watakaozuiliwa wokovu? Ufunuo 22:15.**

_______________________________________________________________________________

*Kila udanganyifu, lau kama kusudi lake ni lipi, umejumuishwa katika amri hii. Twaweza kudanganya kwa kupunga mkono (kuashiria) ama kupepesa, ama kwa kuficha ukweli kwa hiari kwa lengo la kudanganya.*

**13. Amri ya kumi inakataza nini? Kutoka 20:17.**

____________________________________________________________________________

*Tamaa ni mtangulizi wa dhambi nyinginezo, kama vile wizi na uzinzi (Mika 2:2). Hii ilikuwa ndio dhambi ya kwanza ya Hawa (Mwanzo 3:6). Mungu anataka kutulinda na kutufanya kuwa na furaha kwa njia ya sheria Yake.*

## *HITIMISHO*

*Msingi wa sheria ya Mungu ni upendo. Zile amri nne za kwanza zinatuonesha jinsi ya kumpenda Mungu. zile sita za mwisho zinatuonesha namna ya kumpenda jirani yetu. Warumi 13:9.*

**14. Lakini, twawezaje kumtii Mungu iwapo tu wadhaifu sana? Wafilipi 2:13; 4:13.**

____________________________________________________________________________

**15. Je, tunaipata mbingu kwa njia ya matendo ya utiifu? Kusudi la sheria ya Mungu ni lipi? Warumi 3:20, 24.**

____________________________________________________________________________

*Hatuwezi kuipata mbingu kwa njia ya matendo yetu. Wokovu ni kipawa tusichostahili kutoka kwa Mungu. Maasi yetu ya zamani yanatuhukumu, lakini kusudi la ile sheria ni kutuonesha sisi dhambi zetu ili twende kwa Yesu na kumwomba atusamehe na atusaidie kuubadili utaratibu wa maisha yetu. Utii ni kielelezo cha upendo wetu kwa Mungu na kumkubali kwetu Yesu kama Bwana wetu. Yohana 14:15.*

**16. Laiti tukisema pamoja na Paulo, "Bwana, wataka nifanye nini?" (Matendo 9:6) na tumechagua kuzitii amri za Mungu, tutapokea nini?**

*a) Kumbukumbu 28:1, 2, 9, 13.* ________________________________________________

*b) Maombi yetu yatajibiwa (1 Yohana 3:22). Tutakuwa nayo amani ya rohoni (Isaya 48:18), hekima (Zaburi 119:104), afya (Kutoka 15:26), pamoja na maisha marefu (Kumbukumbu 4:40).*

Ili kupokea mibaraka hii yote iliyoahidiwa, je, unakubali kuzitii amri zote za ile Sheria Takatifu ya Mungu kutokana na kumpenda Yesu? Je, unapenda kumwomba Bwana akusaidie kuzishika kwa uaminifu?

---

***Uamuzi wangu:*** *Nataka Mungu anijalie uwezo wa kushika kila moja ya hizi Amri Kumi, kwa njia ya imani.* ◯ *Ndio* ◯ *Hapana*

---